


MKATABA WA MAUZIANO YA ARDHI



KATI YA

Edgard E. Kazimoto

NA



Mary Jimmy Malle

KWA ENEO LILILOPO MAGOLE A KATA YA KIVULE,

MANISPAA YA ILALA, DAR ES SALAAM

UMETAYARISHWA NA:

MARY JIMMY MALLE

P.O BOX 2819

DAR ES ES SALAAM.

MKATABA WA MAUZIANO YA ARDHI

Mkataba huu umefanyika leo tarehe 21 mwezi 02 mwaka 2024

KATI YA

EDGARD E. KAZIMOTO wa KIVULE ambao katika Mkataba huu wanatajwa kama “**MUUZAJI**” (jina ambalo tafsiri yake itajumuisha warithi, wasimamizi wa mirathi na watekelezaji wa wosia wake) kwa upande wa kwanza;

NA

MARY JIMMY MALLE, Wa Kivule, Dar es Salaam, ambaye ndani ya makubaliano haya haya atakua anatajwa kama “**MNUNUZI**” ambapo tafsiri yake itajumuisha mrithi, msimamizi wa mirathi na mtekelezaji wa wosia wake) kwa upande wa pili.

KWA KUWA MUUZAJI ni mmiliki halali wa eneo na maendelezo yote yaliyopo katika eneo lililopo kata ya KIVULE, Manispaa ya ILALA jijini Dar es Salaam lenye ukubwa wa **mita 41x48x40.5x48.80** ambalo lipo KIVULE, katika mkataba huu kitaitwa “**KIWANJA**” ambacho mipaka yake yote imeonyeshwa hapa chini;

NA KWA KUWA MUUZAJI ameamua kumuuzia MNUNUZI kiwanja hicho, kwa mujibu wa masharti yaliyopo katika mkataba huu na kwamba MNUNUZI ameshakagua na kutembelea kiwanja hicho na kuridhika na hali iliyopo katika kiwanja hicho;

NA KWA KUWA MNUNUZI ameonesha nia ya kununua kiwanja hicho katika hali iliyopo katika kiwanja hicho;

HIVYO BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA KAMA IFUATAVYO:

1. KWAMBA MUUZAJI anauza kiwanja hicho kikiwa hakina migogoro yoyote na hakiko chini ya madai yoyote na kwamba umiliki wa MUUZAJI wa kiwanja hicho haugombaniwi wala kubishaniwa na mtu yoyote.

2. Kwamba, mipaka ya kiwanja hicho ni kama inavyoainishwa hapa chini;
 - I. Upande wa Kaskazini kimepakana na **DORA KOTI** na **RAMADHANI RAJABU (41m)**
 - II. Upande wa kusini kimepakana na **BARABARA/RAZAKI ISIHAKA (48m)**
 - III. Upande wa mashariki kimepakana na **BARABARA (40.5m)**
 - IV. Upande wa magharibi kimepakana na **BONDE/KIDULAZI (48.80m)**
3. Kwamba MUUZAJI amekubali kumuuzia kiwanja hicho MNUNUZI kwa kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni Hamsini na tisa na laki tano tu (TZS 59,500,000/=).
4. Kwamba kwa kuweka sahihi mkataba huu, MUUZAJI anakiri kupokea kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni hamsini na tisa na laki tano tu (TZS 59,500,000/-) kutoka kwa MNUNUZI.
5. Kwamba, kwa kupokea kiasi tajwa katika kifungu cha 3, MUUZAJI anamruhusu MNUNUZI kulitumia eneo hilo kwa namna atakavyoona inafaa.
6. Kwamba kwa mkataba huu MUUZAJI anamkabidhi MNUNUZI kiwanja hicho kiwe katika milki yake moja kwa moja na hataingilia umiliki wa MNUNUZI.
7. Kwamba kwa kuweka sahihi katika Mkataba huu, pande zote mbili zitakua zimekubali kutimiza masharti ya Mkataba huu.
8. Kwamba Mkataba huu unaheshimu na kulindwa na sheria za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Endapo upande mmoja kati ya wahusika wa Mkataba huu utashindwa kutimiza masharti ya Mkataba na kusababisha kuvunjika kwa Mkataba huu, shauri hilo litatatuliwa kwa kufuata Sheria za Mikataba kwa mujibu wa Sheria za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

KWA USHUHUDA pande zote mbili katika mkataba huu zimeweka mikono yao na kusaini makubaliano haya siku na tarehe inayoonekana hapa chini:

Imetiwa sahihi na kutolewa na

EDGAR E. KAZIMOTO

Ninaye mfahamu kwa sura au


Aliyetambulishwa kwangu na

MARY JIMMY MALLE ambaye

Namfahamu kwa sura

Leo tarehe ... 21 ... mwezi wa ... 02 ...

Mwaka 2024



MUUZAJI

SHAHIDI;

Jina EVA ALOYCE MMASSE

Sahihi: E. Masse

Anuani: HIVULE DSM.

Wadhifa: MHE.

MBELE YANGU;

Jina Lupakisto Mwambinga

Sahihi: Lupakisto Mwambinga

Anuani: 9393

Wadhifa: WAKILI



Imetiwa sahihi na kutolewa na

MARY JIMMY MALLE

Leo tarehe 21 mwezi wa 02
Mwaka 2024

MNUNUZI

SHAHIDI;

Jina ABUBAKAR KIHDAQUE

Sahihi:

Anuani: 073211727

Wadhifa: M/KITI MTA



MBELE YANGU;

Jina Lupakiso Mwambinga

Sahihi:

Anuani: 9393

Wadhifa: WAKILI

